KATIBA YA UMOJA WA WANACHUO

NLAB INNOVATION ACADEMY STUDENT ORGANIZATION

(NIASO)

MWAKA 2021

UTANGULIZI

Sisi Wanachuo wa Nlab Innovation Academy tumeamua kwa dhati kuwa Wanachuo tunaofuata na kuzingatia misingi ya uhuru,haki na amani.

Na kwa kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia,ambayo Serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na kama chombo kinachowakilisha Wanachuo wote na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za Mwanachuo zinadumishwa na kulindwa na wajibu wa kila mwanachuo unatekelezwa kwa uaminifu.

Kwa hiyo basi katiba hii imetengenezwa na sisi Wanachuo wote kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo na pia kuhakikisha kwamba Wanachuo wanaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora na isiyokuwa na ukabila wala dini.

SURA YA KWANZA

SEHEMU YA KWANZA;

JINA LA CHAMA

1.1. NLAB INNOVATION ACADEMY STUDENTS ORGANISATION (NIASO)

SEHEMU YA PILI

2.1. MADHUMUNI/MALENGO MUHIMU NA MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI

2.1.i) Serikali ya NIASO ni Serikali inayotakiwa kufuata misingi ya demokrasia,haki na utawala bora ,kwa hiyo basi;-

2.1.ii) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni kushiriki katika kupanga mipango mbalimbali ya Chuo na kuratibu ustawi wa Wanachuo.

2.1.iii) Serikali ya NIASO itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa Wanachuo hivyo basi wanachuo ndio misingi wa mamlaka yote kwa mujibu wa katibu hii.

2.1.iv) Serikali ya NIASO itatakiwa kuwa na mahusiano mazuri kati yake na Uongozi wa Chuo na Serkali mbalimbali za Wanachuo za Taasisi nyingine za Mafunzo.

2.2. Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Chuo na Serikali ya Wanachuo kutokana na kufuata misingi ya utawala bora kwa kuzingatia mazingira ya Chuo kwa ujumla.Kwa hiyo Serikali ya Wanachuo inawajibika kuelekeza shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha;-

a. -Utu na haki za Wanachuo zinaheshimiwa na kuthaminiwa

b. -Sheria za Chuo zinalindwa na kutekelezwa
c. -Shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba mali za Chuo zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa manufaa ya Wanachuo na kuzuia mtu/watu kuzitumia vibaya au kwa masilai yao binafsi.
d. -Kwamba maendeleo ya Chuo na Wanachuo yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja.
e. -Kwamba Elimu bora inatolewa kwa Wanachuo wote kwa haki na usawa
f. -kwamba aina yoyote ya vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo vinaondolewa chuoni.
g. -Mfuko wa wanachuo ulindwe na uendelezwe kwa maslahi ya wanachuo wenyewe.

2.3. Vikao vyote vya wanachuo vya ndani nilazima vipate ridhaa au ruhusa kutoka kwa Spika wa Bunge na si vinginevyo. Kiongozi au mwanachuo atakaye bainika kuendesha kikao chochote bila ruhusa ya Spika wa Bunge hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kulingana na katiba hii.

2.4. UTARATIBU NA MATUMIZI YA MFUKO WA NIASO.

2.4.i) Fedha zitatolewa au kuwekwa benki kwa saini zifuatazo;

a) Mlezi na Msimamizi taratibu za fedha za chuo (Mhasibu wa chuo)

b) Rais wa serikali ya wanachuo (NIASO)

c) Waziri wa fedha wa serikali ya wanachuo (NIASO)

2.3.ii) Serikali ya wanachuo (NIASO) itagharamikia gharama zote na shughuli zote za chama ambazo mjumbe atakazokuwa ametumwa na kufanya kwa maslahi ya wanachuo, si vinginevyo.

2.3.iii) Matumizi ya fedha kiasi chochote yapate ridhaa kutoka kwenye kikao cha Bunge.

2.3.iv) Suala la ubadhirifu wa aina yoyote kuhusu fedha za chama itapelekwa katika kamati ya Bunge katiba,sheria na nidhamu na hatua kuchukuliwa kulingana na taratibu za katiba hii.

SEHEMU YA TATU;

3.1. MASHARTI YA UANACHAMA

3.1.i) Kila Wanachuo atakapojiunga na Chuo atakuwa mwanachama wa NIASO moja kwa moja.

3.1.ii) Kila mwanachama anatakiwa kulipa Tshs.10,000 kama ada ya Uanachama Kwa mwaka

3.1.iii) Mwanachama anatakiwa kuhudhuria vikao vyote vitakavyoitishwa na Serikali.

3.1.iv) Mwanachama yeyote anatakiwa kuheshimu serikali iliyopo madarakani na serikali imweshimu mwanachama.

3.1.v) Utovu wa nidhamu kwa Serikali au viongozi hatua za kinidhamu zitachukuliwa kulingana na kanuni na taratibu na Sheria za Chuo.(kupitia kamati ya Bunge ya Nidhamu).

3.1.vi) Wanachuo wote watashiriki katika shughuli zote za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya katiba hii.

3.1.vii) Malalamiko yote yapitie katika ngazi zinazohusika na si vinginevyo.

3.1.viii) Kila mwanachuo atachangia michango itakayo kubalika na wajumbe zaidi ya nusu watakao hudhuria mkutano wa wanafunzi wote.

SURA YA PILI

UONGOZI WA SERIKALI YA NIASO

SEHEMU YA NNE;

4.1. SIFA/MAADILI YA KIONGOZI

4.1.a) Awe mwanachama hai wa NIASO.

4.1.b) Awe mwadilifu.

4.1.c) Awe mwaminifu.

4.1.d) Afuate Katiba ya NIASO ,Sheria na Kanuni za Chuo.

4.1.e) Akubali kukosolewa katika kikao cha viongozi.

4.1.f) Awe na uwezo wa kuongoza na kimasomo(darasani)

SEHEMU YA TANO;

5.1. MGAWANYO WA MAJUKUMU KATIKA SERIKALI YA NIASO.

5.1.A. RAIS WA SERIKALI YA NIASO.

5.1. (i) Kutakuwa na Rais wa Wanachuo ambaye atatangazwa kuwa Rais iwapo tu amepata kura nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yeyote.

5.1.(ii) Rais wa Serikali ya Wanachuo.

5.1.(iii) Kusimamia maamuzi na shughuli zote zinazohusu Wanachuo.

5.1.(iv) Kuongoza Shughuli zote za Serikali ya wanachuo (NIASO).

5.1.(v) Atakuwa mweka saini wa kwanza Benki.

5.1.(vi) Kushauri Uongozi wa Chuo juu ya masuala ya maslahi ya Wanachuo.

5.1.(vii) Mjumbe wa kamati ya Taaluma.

5.1.(viii) Mjumbe wa kamati ya Rufaa ya nidhamu.

5.1.(ix) Mjumbe wa kamati ya Mahafali.

5.1.(x) Rais anamamlaka ya kuunda na kufuta baraza la mawaziri na bunge (NIASO) bila kuathiri taratibu na kanuni za katiba hii.

5.1.(xi) Katiba na sheria inamruhusu Rais kutumia utashi wake mwenyewe kuchukuwa maamuzi kuiongoza serikali ya wanachuo bila kufungwa na ushauri alio upata kutoka kwa mtu au mamlaka yeyote ile isipokuwa tu kama katiba au sheria inamtaka afanye hivyo.

5.1.(xii) Rais anamamlaka ya kutoa msamaha kwa mwanachuo mwenye kosa lisilo la jinai.

(Kwa kuomba uongozi wa chuo au kamati ya nidhamu)

5.1.B. MAKAMU WA RAIS NIASO

5.1.(i) Kutakuwa na Makamu wa Rais ambaye atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Serikali ya Wanachuo na hususani;-

5.1.(ii) Atamsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa siku hata siku wa mambo yote.

5.1. (iii) Atafanya kazi zote atakazoagizwa na Rais.

5.1.(iv) Atafanya kazi zote za Rais kama Rais hayupo.

5.1.(v) Mjumbe wa kamati ya Nidhamu ya Chuo.

5.2. UTEUZI

5.2.(i) Makamu wa Rais atapatikana kwa kuchaguliwa katika uchaguzi uleule kwa pamoja na Rais na watapigiwa kura kwa pamoja .Mgombea kiti cha Urais akichaguliwa basi na Makamu wa Rais atakuwa amechaguliwa.

5.2.(ii) Rais wa NIASO anamamlaka kamili kuteua,kuwaondoa madarakani watendaji wakuu wafuatao;-

5.2. a.Waziri mkuu.

5.2. b.Mawaziri na manaibu waziri.

5.2.c.Mbunge atakayethibitishwa na Bunge kama utendaji wake hauna tija wala maslahi kwa wanachuo(Jimbo lake) au Chuo.

5.2.(iii) Kamati ya Bunge nidhamu,katiba,sheria na maadili inamamlaka kamili ya kuchagua na kuteua kamati/tume ya uchaguzi wa Serikali ya NIASO.

SEHEMU YA SITA.

6.1 WAZIRI MKUU, BARAZA LA MAWAZIRI NA SERIKALI

6.1.A. WAZIRI MKUU (NIASO)

6.1.(i) Kutakuwa na Waziri Mkuu wa Serikali ambaye atateuliwa na Rais, kutoka ndani au nje ya Bunge na kabla ya kuapishwa na kushika madaraka atapigiwa kura za kukubaliwa na Bunge.

6.1.(ii) Atakuwa na madaraka juu ya udhibiti,usimamizi,utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya wanachuo (NIASO).

6.1.(iii) Atakuwa msimamizi /kiongozi wa shughuli za Serikali(NIASO) Bungeni.

6.1.(iv) Kutekeleza jambo/mambo ambayo ataagizwa kutekeleza na Rais/Bunge.

6.1.(v) Kusimamia na kutekeleza shughuli zote zinazo hitajika kwa Bunge(Wabunge).

6.1.(vi) Kuhakikisha na kutunza kumbukumbu zote za Serikali ya wanachuo (NIASO).

6.1.(vii) Atakuwa Katibu wa Baraza la Mawaziri.

6.1.B. BARAZA LA MAWAZIRI NIASO.

6.1.(i) Kutakuwa na Baraza la Mawaziri ambalo wajumbe wake watakuwa ni Rais,Makamu wa Rais,Waziri Mkuu na Mawaziri wote na Manaibu.

6.1. (ii) Rais ataongoza mikutano yote ya Baraza la Mawaziri.

6.1.(iii) Mawaziri wote watateuliwa na Rais na Makamu wa Rais kwa kushauriana na Waziri mkuu.

6.1. (iv) Mawaziri wote na Manaibu watachaguliwa kutoka miongoni mwa wabunge au nje ya Bunge lakini kwa kuzingatia usawa kwa kila kozi.

6.1. (v) Waziri au naibu atashika madaraka yake baada ya kuapa kwanza mbele ya Rais kiapo cha uaminifu.

6.1.(vi) Mawaziri na Manaibu watatakiwa kuandaa/kuunda mipango na kuunda bajeti katika Wizara zao na kuziwakilisha kwa Bunge kwa ajili ya kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

SEHEMU YA SABA.

7.1 BUNGE LA NIASO

7.1.(i) Kutakuwa na Bunge la Wanachuo ambalo litakuwa na sehemu mbili yaani Rais na Wabunge.

7.1. (ii) Rais atakuwa sehemu moja ya Bunge.

7.1. (iii) Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Serikali ya(NIASO) ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya Wanachuo,kuisimamia na kuilinda Serikali ya (NIASO) katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa katiba hii.

7.1.(iv) Wabunge watachaguliwa kutoka katika Majimbo na watakuwa Wawakilishi wa Madarasa na Hostel kwa upande wa Chuo kwa mujibu wa katiba hii.

7.1.(v) Kila kiongozi anapaswa kuheshimu serikali iliyopo madarakani kwa mujibu wa katiba hii.

7.2. Madhumuni na Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ni kama;-

7.2.(i) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa BUNGE.

7.2. (ii) Kujadili mipango mbalimbali iliyopangwa na Mawaziri

7.2. (iii) Kujadili matumizi na kuidhinisha fedha kutoka kwenye mfuko wa (NIASO).

7.2.(iv) Waziri yeyote ataulizwa swali lolote kuhusu mambo ambayo yako katika wizara yake.

7.2.(v) Kujadili Bajeti zilizopangwa na Mawaziri wa kila Wizara.

7.2. (vi) Wabunge watakuwa wajumbe wa kamati ya Nidhamu kutoka jimbo husika.

7.2.(vii) Kamati za Bunge zitatambulika kwa uongozi wa chuo na zitatoa maamuzi kwa jambo lolote linalo muhusu mwanachuo kabla ya uongozi wa chuo.

7.2.(viii) Madaraka na majukumu ya Mbunge katika jimbo lake;

a) Kuhakikisha na kumkumbusha mwalimu anaingia na kufundisha kwa muda ulio pangwa.

b) Kutoa taarifa juu ya matatizo ya kidarasa katika uongozi unaostahili.

c) Kutoa taarifa za wanafunzi wenzake kwa mwalimu iwapo ni mgonjwa au anamatatizo mengine.

d) Kusimamia na kutunza vitu vilivyoko darasani.

e) Kuhakikisha madarasa yako safi.

7.3. WABUNGE, MAJIMBO YA UCHAGUZI NA UCHAGUZI WA WABUNGE.

7.3.(i) Kutakuwa na aina zifuatazo za Wabunge;

7.3.a) Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha majimbo ya Uchaguzi.

7.3.b) Mawaziri na Manaibu Mawaziri ambao watateuliwa na Rais ambao hawakugombea Ubunge watakuwa wabunge moja kwa moja baada ya kuchaguliwa kuwa Mawaziri.

7.3.c) Spika wa Bunge atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge au nje ya Bunge.

7.3.ii. Wabunge wote wa aina zote watashika madaraka yao kwa mujibu wa katiba hii na watalipwa posho Tsh.5000/= kwa kila kikao katika vikao (5) vya Bunge kwa semista na katika shughuli zinginezo.

7.3.iii. Kuwakilisha matatizo ya majimbo (madarasa) kwa uongozi wa husika.

7.3.iv. Anahaki ya kuhoji jambo analoliona linaenda kinyume endapo tu atapata ruhusa kutoka kwa Spika.

7.3.v. Mbunge anahaki ya kuomba mwongozo wakati Mbunge akiendelea kuongea, na Spika atakua na haki ya kumruhusu au kukataa kwa maslahi ya(NIASO).

7.3.vi. Mbunge/Waziri anahaki ya kuomba utaratibu kutokana na hali ya Bunge ilivyo kwa mfano haina utulivu,haki imepotea na mengine kama hayo, Spika anamamlaka ya kumruhusu au kutokumruhusu na Spika akaiweka hali sawa.

7.3.vii. Spika anamamlaka ya kumwajibisha kiongozi yeyote atakaye onesha utovu wa nidhamu ndani ya Bunge kwa mfano kuongea lugha ya matusi, kashfa na mengine kama hayo.

7.3.viii. Spika ndiye mwenyemaamuzi ya mwisho Bungeni au yeyote atakaye kabidhiwa kiti cha Spika siku hiyo (kwenye kikao cha Bunge).

SEHEMU YA NANE.

8.1 MAJIMBO YA UCHAGUZI

8.1.i) Kutakuwa na majimbo ya uchaguzi ambayo ni kila kozi Madarasa kwa mwaka wake kwa chaguzi za Wabunge na hostel.

8.1.ii) Majimbo yenye watu zaidi ya 50 yatatoa Wabunge 2 na chini ya hapo yatatoa mbunge mmojammoja kwa kila jimbo.

8.1.iii) Kutakuwa na kituo kimoja cha kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu kama itakavyo pangwa na tume ya uchaguzi.

8.2 UCHAGUZI MKUU.

8.2.i) Uchaguzi mkuu utafanyika kila baada ya mwaka mmoja ili kupata Serikali mpya.

8.2.ii) Wanachuo wote watakaotaka kugombea Uongozi watatakiwa kujaza fomu kwa gharama itakayopendekezwa na kamati/Tume husika, kugombea nyadhifa mbalimbali zitakazogombewa.

8.3 TUME YA UCHAGUZI

8.3.i) Kamati ya Bunge nidhamu,katiba,sheria na maadili itachagua wajumbe watakaounda tume ya Uchaguzi.

|8.3.ii) Tume ya uchaguzi itakuwa na wajumbe wasiozidi kumi(10)

8.3.iii) Wajumbe wanaohusika na Tume ya Uchaguzi ni;-

8.3.a) Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi.

8.3.b) makamu mwenyekiti

8.3.c) wajumbe

8.3.iv) Tume ya Uchaguzi itafanya kazi kwa usimamizi wa Idara ya Mafunzo chini ya mwalimu mlezi(ssw).

8.3.v) Kamati ya Bunge nidhamu,katiba,sheria na maadili inamamlaka ya kumuhoji na kuhakikisha kiongozi anayegombea uongozi anafaa kwa maslahi ya (NIASO) na chuo kwa ujumla.

8.4 UCHAGUZI MDOGO

8.4.i) Uchaguzi mdogo utafanyika iwapo kiongozi atashindwa masomo,kujiuzulu,kuachishwa masomo,uongozi au kufariki dunia.

8.4.ii) Pindi kiongozi anapoachishwa uongozi kwa kukiuka taratibu za Chuo na Uongozi.

8.4.iii) Waziri mkuu ndiyo atakaye simamia(mwenyekiti) chaguzi zote ndogondogo.

8.5 RUFAA

8.5.i) Unapotokea utata wowote kwenye uchaguzi mdogo au uchaguzi mkuu tume haitafungwa na kanuni au sheria yoyote kutoa maamuzi.

8.5.ii) Mgombea anaweza kukata rufaa baada tu ya kuona haki,usawa na sheria haikuzingatiwa na tume huru ya uchaguzi kwa SSW kwa muda wa saa 48 baada ya matokeo kutangazwa.

8.5.iii) Rufaa itakatwa nakukubalika pale tu kabla ya Rais/kiongozi aliyechaguliwa kuapishwa.

SEHEMU YA TISA;

9.1 UTARATIBU,MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE

9.1.A SPIKA WA BUNGE (NIASO).

9.1.i) Kutakuwa na Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni wa Waliochukua fomu kuwania nafasi hiyo yaani miongoni mwa wabunge au nje ya bunge mwenye sifa za kuwa kiongozi.

9.1.ii) Atakuwa kiongozi wa Bunge na atawakilisha Bunge katika shughuli na vikao vingine vyote ndani ya Bunge.

9.1.iii) Atachaguliwa kwa kupigiwa kura na Bunge (wabunge), ili aweze kutangazwa mshindi ni lazima awe na kura zaidi ya 50% ya wabunge wote walioshiriki uchaguzi.

9.1.iv) Anamamlaka ya kumtoa mbunge yeyote/kiongozi yeyote atakaye onesha utovu wa nidhamu ndani ya Bunge/kikao.

9.1.v) Anamamlaka ya kuzuia kiongozi yeyote kuhudhuria vikao vya bunge visivyozidi viwili kutokana na makosa kama; kutotii amri ya Spika,kudharau kwa kutoa lugha ya kashfa kwa Bunge,mawaziri au Rais na makosa kama hayo, nk.

9.1.vi) Atapanga na kuzisimamia kamati za Bunge.

9.1.vii) Spika anamamlaka ya kuchagua kiongozi (Mbunge/Waziri) kukaimu nafasi yenye mapungufu ndani ya Bunge.

9.1.viii) Ni msemaji wa mwisho Bungeni.

9.1.B. NAIBU SPIKA WA BUNGE

9.1.i) Atafanya kazi zote za Spika kama Spika hayupo.

9.1.ii) Atakuwa mshauri mkuu wa Spika katika kuteuwa kamati za Bunge na kutoa maamuzi ya busara/hekima Bungeni.

9.1.iii) Atachaguliwa pamoja na Spika katika uchaguzi mkuu ndani ya Bunge.

9.1.iv) Atakuwa msemaji wa mwisho Bungeni kama Spika hayupo.

9.2. Spika atakoma kuwa spika na ataacha kiti cha Spika litakapotokea lolote kati ya mambo yauatayo;-

9.2.a) Atachaguliwa kuwa waziri.

9.2.b) Endapo itathibitika kuwa amevunja masharti ya sheria inayohusu maadili ya viongozi wa serilikali ya (NIASO)

9.2.c) Endapo atajiudhuru madaraka ya Spika.

9.2.d) Spika ataacha kuwa Spika endapo tu Bumge litakuwa halina imani naye kwa nusu ya Wabunge.

9.2.e) Endapo atafariki dunia,ataacha chuo,atafukuzwa chuo.

9.3. WAJIBU WA CHUO KWA SERIKALI YA WANACHUO (NIASO).

9.3.i) Chuo kitakuwa ni mlezi mkuu wa serikali ya wanachuo.

9.3.ii) Chuo kitatoa asilimia 30 (30%) ya fedha katika mfuko wa wanachuo, 15% semester ya kwanza na 15% semester ya pili.

9.3.iii) Muhasibu wa chuo atakuwa mkaguzi mkuu wa matumizi ya mfuko wa fedha za wanachuo .

SURA YA TATU.

MAJUKUMU KWA BARAZA LA MAWAZIRI KWA KILA WIZARA NA MIPAKA YAKE (MWONGOZO KWA WIZARA HUSIKA);

1. WIZARA YA ELIMU.

1.a WAZIRI WA ELIMU.

1.a.i) Atafanya kazi ya kuhakikisha walimu wanatimiza wajibu wao wa kufundisha na kumaliza module zao.

1.a.ii) Take home na test (class assessment) zitolewe kuendana na kile kilicho fundishwa.
1.a.iii) Awemsikivu pale anpopelekewa malalamiko kuhusu Elimu.

1.a.iv) Apitie attendance zote kuhakikisha mahudhurio ya Wanachuo kwa kuridhia 75% na mwanafunzi au 100%.(Apate ushirikiano kutoka kwa Mbunge husika).

1.a.v) Awasaidie wanachuo wanao shindwa kupata ufaulu unaostahili (walio fail) waweze kupewa nafasi nyingine ya kufanya mtihani (test/assignment) au make up.

1.a.vi) Ni mjumbe wa kamati ya chuo ya nidhamu ya Wanafunzi.

1.a.vii) ni msemaji wa mwisho katika wizara yake.

1.b NAIBU WAZIRI WA ELIMU.

1.b.i) Atafanya kazi zote kwa ushirikiano na Waziri wake.

1.b.ii) Atafanya kazi zote na kuwajibika katika wizara endapo waziri hatakuwepo mazingira ya kazi/chuo.

1.b.iii) Atakuwa mshauri mkuu kwa waziri wake katika kutoa maamuzi ya wizara.

2. WIZARA YA KATIBA ,SHERIA NA NIDHAMU.

2.a WAZIRI WA KATIBA,SHERIA NA NIDHAMU.

2.a.i) Atasaidia kutoa ufafanuzi wa sheria ndani ya serikali inapo pata mkanganyiko wa kisheria au katiba.

2.a.ii) Atamwajibisha mwanafunzi yeyote atakaye enda kinyume (vunja) cha kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa katiba na sheria za (NIASO) na Chuo kwa ujumla.

2.a.iii) Awetayari kupokea mawazo/maoni ya wanachuo na Walimu.

2.a.iv) Asimamie haki za wanachuo kwa mujibu wa sheri na taratibu.

2.a.v) Ashauriane na kamati ya Bunge ya katiba,sheria na nidhamu kwa maamuzi mazito.

2.a.vi)Ni msemaji wa mwisho katika wizara yake.

2.b NAIBU WAZIRI WA KATIBA,SHERIA NA NIDHAMU.

2.b.i) Atafanya kazi zote za wizara kwa ushirikiano na waziri.

2.b.ii) Atafanya kazi zote endapo waziri hatakuwepo mazingira ya kazi au chuo.

2.b.iii) Amwombe ushauri waziri wake.

3. WIZARA YA FEDHA,UCHUMI NA MIPANGO.

3.a. WAZIRI WA FEDHA,UCHUMI NA MIPANGO.

3.a.i) Ni msimamizi wa fedha(NIASO-ACCOUNT) zinazo changwa na wanafunzi (wanachuo).

3.a.ii) Awe mbunifu (creative) juu ya kutunisha mfuko wa wanachuo.

3.a.iii) Ahakikishe fedha inatumika kwa manufaa ya wanachuo.

3.a.iv) Awetayari kupokea mawazo ya wadau/wanachuo.

3.a.v) Ni mweka saini benki.

3.a.vi) Awe na idadi kamili ya walipaji au wanachama wa NIASO.

3.a.vii) Awe na uwezo wa kusimamia msimamo wake kwa maslahi ya wanachuo/NIASO.

3.a.viii) Awe na kumbukumbu za mapato na matumizi kwa kila fedha iingiayo na kutoka na kuzitolea taarifa kwa wanachuo.

3.a.ix) Ni msemaji wa mwisho katika wizara yake.

3.b. NAIBU WAZIRI WA FEDHA,UCHUMI NA MIPANGO.

3.b.i) Ni mshauri/ashauriane na waziri wake kuhusu ubunifu wa mipango na uendeshaji wa wizara.

3.b.ii) Atafanya kazi zote endapo waziri wake hatakuwepo eneo la kazi, isipokuwa uwekaji wa saini benki.

3.b.iii) Awe na kumbukumbu zote za fedha zinazotoka na kuingia.

4. WIZARA YA AFYA,CHAKULA NA MAZINGIRA.

4.a WAZIRI WA AFYA,CHAKULA NA MAZINGIRA.

4.a.i) Ahakikishe chakula kinachotolewa na mzabuni kinaubora wa kutosha.

4.a.ii) Maeneo ya chuo yote kwa ujumla wake yanakuwa safi kwa wakati wote.

4.a.iii) Ashirikiane na waziri wa fedha ili awezekupata fedha kwa ajili ya kununua vifaa kama vile madawa ya kutuliza maumivu na kwa ajili ya mambo mengine.(emergency)

4.a.iv) Kuwa na idadi kamili ya wanafunzi wanao lala/ishi hostel.

4.a.v) Awe na kumbukumbu ya vitu/matukio yote yanayohusu hostel.

4.a.vi) Ni mtoa taarifa za wagonjwa na wenye matatizo ya kudumu.

4.a.vii) Nimsemaji wa mwisho wa wizara yake.

4.b NAIBU WAZIRI WA AFYA,CHAKULA NA MAZINGIRA.

4.b.i) Washirikiane kwa kazi zote na waziri wake.

4.b.ii) Ni mtoaji wa taarifa za wangojwa na mazingira kwa ujumla kwa waziri wake.

4.b.iii) Atawajibika kwa kila kitu endapo waziri hayupo eneo la kazi au chuo.

5. WIZARA YA HABARI NA MAWASILIANO.

5.a. WAZIRI WA HABARI NA MAWASILIANO.

5.a.i) Atatoa habari iliyo tayari kwa maelekezo ya Rais,Waziri au Spika.

5.a.ii) Awe tayari kutumwa kwa faida ya (NIASO),Chuo na wanachuo kwa ujumla.

5.a.iii) Atumie utashi wake kutoa habari zinazo jenga mara zote na siyo za kubomoa.

5.a.iv) Atoe habari kwa muda muafaka pale anapoagizwa.

5.a.v) Atumie lugha nzuri na rahisi/nyepesi ili kila mmoja aelewe ujumbe.

5.a.vi) Awe mbunifu na ashirikiane na vyanzo vingine vya habari.

5.a.vii) Ni msemaji wa mwisho katika wizara yake.

5.b. NAIBU WAZIRI WA HABARI NA MAWASILIANO.

5.b.i) Amshauri vizuri waziri wake.

5.b.ii) Atafanya kazi zote za waziri endapo waziri hata kuwepo.

5.b.iii) Amsaidie waziri kubuni njia nzuri za mawasiliano na uongozi wa chuo na serikali ya wanachuo.

6. WIZARA YA MICHEZO NA UTAMADUNI.

6.a WAZIRI WA MICHEZO NA UTAMADUNI.

6.a.i) Ahakikishe anapanga vizuri ratiba ya michezo walau kila wiki mechi ya ndani.

6.a.ii) Ahakikishe ratiba ya michezo inafuatwa.

6.a.iii) Ahakikishe michezo haivunji maadili ya chuo na nchi kwa ujumla.

6.a.iv) Awe na usawa wa michezo isipendelee jinsia moja.

6.a.v) Ashirikiane na vyuo/taasisi nyingine ilituweze kupata mechi nyingi zaidi za nje.

6.a.vi) Ahakikishe zawadi ziwe na tija kwa washindi na zitolewe kwa wakati muafaka na izingatie aina ya mchezo na washiriki wake.

6.a.vii) Ahakikishe nidhamu inazingatiwa na watovu wa nidhamu wanashughulikiwa.

6.a.viii) Ndiye atatakiwa kutunza vifaa vya michezo.(Tv na DSTV,Sare za michezo na n.k)

6.a.ix) Kufuatilia shughuli zote zinazo husiana na michezo, burudani na starehe.

6.a.x) Ni msemaji wa mwisho wa wizara yake.

6.b. NAIBU WAZIRI WA MICHEZO NA UTAMADUNI.

6.b.i) Ashirikiane na waziri kufanya,kupanga shughuli zote za michezo katika wizara.

6.b.ii) Atafanya kazi zote za waziri endapo waziri hayupo kazini au chuo.

6.b.iii) Awe mshauri wa waziri wakati wote wa utendaji.

7. WIZARA YA ULINZI NA USALAMA.

7.a. WAZIRI WA ULINZI NA USALAMA.

7.a.i) Ahakikishe ulinzi katika mali ya wanachuo inalindwa kwa kushirikiana na ofisi ya Rais wa NIASO.

7.a.ii) Atumie busara kutatua matatizo,migogoro,ugomvi au fujo pindi inapotokea.

7.a.iii) Asiwe mtu wa kuanzisha/kuchochea migogoro,ugomvi/migomo.

7.a.iv) Asisite kumchukulia mtu yeyote hatua za kinidhamu pale anapo vunja sheria.

7.a.v) Kwa maamuzi mazito ya kinidhamu ashauriane na kamati ya Bunge sheria,katiba na nidhamu.

7.a.vi) Ni msemaji wa mwisho kwenye wizara yake.

7.b. NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA USALAMA.

7.b.i) Ashirikiane na waziri kupanga na kufanya kazi zote na utendaji.

7.b.ii) Atafanya kazi zote za waziri endapo waziri hatakuwepo eneo la kazi au chuo.

7.b.iii) Awe tayari kupokea ushauri na amwombe waziri ushauri katika utendaji wa kazi.

8.1. MAKABIDHIANO.

8.1.i) Viongozi wote watalazimika kukabidhi ripoti na vifaa mbalimbali ikiwemo mafaili ya kumbukumbu kwa Rais wa serikali ya wanachuo (NIASO) mbele ya kikao cha Bunge. Rais anayemaliza muda wake, atamkabidhi Rais mpya aliyechaguliwa na wanachuo mali na vafaa vyote vilivyopo chini ya ushahidi wa tume ya uchaguzi.

WANACHUO (NIASO)